


AHLUL BAYT

Ni Nani, Si Nani

Abdilahi Nassir

AHLUL BAYT

NI NANI, SI NANI

Kimeandikwa na:

Abdilahi Nassir

Haki ya kunakili imehifadhiwa na
Abdilahi Nassir, 2008

Chapa ya Kwanza 2013

Kinatangazwa na
MARKAZI YA AHLUL BAYT
S.L.P. 84603-80100
MOMBASA (KENYA)

Simu: +254 723 701170

YALIYOMO

Utangulizi i

Chanzio 1

Hujja Zetu 2

Hadith Tulizozitegemea Sisi 6
- Sampuli Chache 6
- Maswahaba 7
- Maimamu wa Wapokezi wa Hadith 8
- Vitabu vya Hadith 9
- Vitabu vya Tafsiri ya Qur'ani 9
- Tunavyojifunza 10
- Sheikh Mazrui Hakubali! 11

Hujja Zake 12
- Sibaaq na Siyaaq 14
- Kanuni za Kiusuli 19
- Hujja ya Kilugha 22
- Tunavyosema na Tusivyosema 26
- Kiini cha Mjadala Wetu 28
- Matumizi ya Maneno Katika Lugha 31
- Kujeruhi Sanad 32

Wake wa Mtume Wamo? 33
- Riwaya Wanazozitegemea 33
- Ibn Abbas 33
- Ikrimah 34
- Urwa b. Zubayr 35
- Muqatil b. Sulayman 36

Tuliyoyajadili Humu kwa Mukhtasari 37

UTANGULIZI

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote. Na rehema na amani zimshukie Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w.) na aali zake, na wote wenye kuwaandama wao hadi Siku ya Malipo.

Hiki ni kitabu chectu cha pili, baada ya kile cha *Hadith al-Thaqalayn: Hadith Sahihi*, tunachokitoa katika mfululizo wa vitabu vyetu kadha kuyajibu aliyoyaandika Sheikh Juma Mohammad Al-Mazrui katika kitabu chake alichokiita *Al-Qistasu Al-Mustaqim: Mezani ya Haki*.

Katika kitabu hiki tunayajibu yake alivyoyaandika Shekhe wetu huyo katika Sura ya Tatu na ya Nne ya kitabu chake hicho (uk. 43-114) ya kudai kwamba muradi wa neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 ni "wake wa Mtume (s.a.w.w.)" **si** "ahlul kisaa", kama tulivyoshikilia sisi mashia bali na *jumhur* ya wanavyuoni wa Kisunni. Tumeanza kwa kutoa hujja zetu za kuthubutisha msimamo wetu, na kumalizia kwa kujibu hujja zake *zote* alizozitoa kukatalia hujja zetu.

Hujja ambayo hatukujishughulisha kujibu, kama tulivyojishughulisha kujibu katika uk. 13-39 wa kitabu chetu cha kwanza, ni ile ya kujeruhi sanad za Hadith zinazotilia nguvu tafsiri yetu ya neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33. Hatukujishughulisha kujibu hujja hiyo kwa sababu niliyoitoa humu (uk. 32).

Abdillahi Nassir

Mombasa
Kenya
19 Muharram 1435AH
23 Novemba 2013

CHANZIO

Katika Qur'ani Tukufu mna sura iitwayo *al-Ahzaab*. Hii ni sura ya 33. Katika sura hii mna aya ya 33 inayosema hivi: "Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea nyinyi uchafu, watu wa nyumba ya Mtume, na kuwatakasa kabisa kabisa." Neno *ahlul bayt* lililomo katika aya hii - ambalo wafasiri wa Qur'ani hulifasiri kwa *watu wa nyumba ya Mtume* – ndilo msingi wa mjadala wetu sisi (mashia) na Sheikh Juma Mohammad al-Marzui.

Sisi mashia tunasema kwamba makusudio ya neno *ahlul bayt* **katika aya hiyo** ni yeye mwenyewe Mtume (s.a.ww.), Sayyidna Alii (a.s.), Bibi Fatimah (a.s.), Sayyidna Hasan (a.s.) na Sayyidna Hussein (a.s.); **sio wake wa Mtume (s.a.w.w.)**. Msemo huu *unakubaliwa na hata baadhi ya wanavyuoni wakubwa wakubwa wa kisunni*, kama tutakavyo ona humu (uk. 8-9) baadaye. Kwa msemo huo, au tafsiri hiyo, tunazo hujja zetu ambazo tumezidondoa humu (uk. 2-11).

Kwa upande wake, Sheikh Mazrui - katika kitabu chake anachokiita *Al-Qistasu Al-Mustaqim* (Mezani ya Haki) – amezipinga hujja hizo kwa urefu sana, kuanzia uk. 44 hadi uk. 117 – hujja ambazo nasi, kwa upande wetu na kwa urefu vile vile, tunazijibu humu kuanzia uk. 17 hadi uk. 47.

Inshallah baada ya kuzisoma na kuzizingatia hujja zake na zetu, ndugu msomaji, utaweza kujiamulia la haki ni lipi.

Ewe Mola! Tuoneshe haki kuwa ni haki, uturuzuku kuifuata; na tuoneshe batili kuwa ni batili, uturuzuku kuipuka. Amin.

HUJJA ZETU

Katika kuitetea tafsiri yetu na kuikataa ya Sheikh Mazuri, tumetegemea hujja k.w.k ambazo ninazidondoa hapa chini:

Hujja yetu ya kwanza ni kwamba hivi tunavyolifasiri sisi neno *ahlul bayt* katika aya hii (Sura 33:33) **ndivyo lilivyofasiriwa na yeye mwenyewe Bwana Mtume (s.a.w.w.)**. Hilo utaliona katika Hadith zake k.w.k zilizo sahihi na mashuhuri (*mutawatir*) zilizopokewa kwa maswahaba wasiopungua ishirini, na kunukuliwa na wanavyuoni wakubwa wakubwa wa Hadith **walio masunni** ambao baadhi yao tumewataja humo (uk. 8-9) pamoja na majina ya vitabu vyao.

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amempa *yeye* Mtume (s.a.w.w.) *kwanza* jukumu la kuifasiri na kuifafanua Qur'ani (Sura 16:44), kisha akatwambia na sisi nasi wafuasi wake, kwamba lolote tunalopewa na yeye tuchuke (Sura 59:7), wala tusiwe na khiari ya kulikataa (Sura 33:36), kwa sababu yeye hasemi kwa matamanio yake isipokuwa husema yale aliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu (Sura 53:3-4); kwa sababu zote hizi ni wazi kwamba panapothubutu tafsiri ya Mtume (s.a.w.w.) - kama ilivyothubutu kuhusu maana ya neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 – hapana nafasi ya tafsiri ya yoyote mwengine, **awe awaye!** Na hilo limekubaliwa na maulamaa wakubwa wakumbwa!

Hujja yetu ya pili ni kwamba Bwana Mtume (s.a.w.w.) hakutosheka na kusema kwa mdomo tu kuwa muradi wa neno *ahlul bayt* katika hiyo Sura 33:33 ni hao watu watano tuliokwisha kuwataja humu (uk. 6-7), **bali alilithibitisha hilo kwa kitendo pia:** kile cha kuipitia nyumba ya Imam Alii (a.s.) na Bibi Fatima (a.s.) mara k.w.k.[1] kila alfajiri alipokuwa akenda msikitini, na kuwanadia: "Swalaa! Enyi *ahlul bayt*!

1 Riwaya ya Bwana Mtume (s.a.w.w.) kupitia nyumba ya Imam Alii (a.s.) na Bibi Fatima (a.s.) na kuwanadia swala hivyo zimenukuliwa katika vitabu vingi vya Tafsir na Hadith kama vile *Tafsir Twabari, Suyuutwi, Sunan Tirmidhi, Mustadrak al-Hakim, Musnad Ahmad* na vinginevyo.

Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu nyinyi *ahlul bayt*, na kuwatakasa kabisa kabisa."

Suali yetu hapa ni: Kama muradi wa neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 ni "wake wa Mtume (s.a.w.w.)", kama anavyodai Sheikh Marzui katika kitabu chake, kwa nini Bwana Mtume (s.a.w.w.) hakuzipitia nyumba za wakeze - na walikuwa nazo zao (tiz. Sura 33:33 na 34) – na kuwanadia hivyo? Bali hakuipitia hata nyumba ya Bibi Ummu Salamah ambamo ndimo mlimoteremshwa[2] aya hiyo?! Kwa nini? Twataraji Sheikh Mazrui atatujibu hilo.

Hujja yetu ya tatu ni kwamba usahihi wa Hadith zinazoifasiri aya hii, *hivi tunavyoifasiri sisi*, umekubaliwa na idadi kubwa ya wanavyuoni wa Hadith (wasio mashia): ama kwa kuitoa katika *sihah* (vitabu vya Hadith sahihi) zao, au kwa kutasua (kuainia) khaswa kuwa ni sahihi. Majina ya wanavyuoni hao na vitabu vyao utayapata uk. 8-9 humu.

Wake wa Mtume (s.a.w.w.) hawamo!

Ama kwa nini tunakataa kwamba wake wa Mtume (s.a.w.w.) ndio waliokusudiwa kwa neno *ahlul bayt* katika hiyo Sura 33:33, tuna hujja ya ziada vile vile.

Hujja hiyo ni ile ya maneno ya riwaya mbili zilizopokewa kwa wake wawili wa Bwana Mtume (s.a.w.w.): Bibi Ummu Salamah na Bibi Aisha. Wao wenyewe wamesema hivi:

1. "Imepokewa kwa Ummu Salamah kuwa: 'Nyumbani mwangu imeshuka (aya ya): *Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea nyinyi uchafu, ahlul bayt...*' Kisha akasema 'Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akatuma aitiwe Alii, Fatima, Hasan na Husein, akasema: *Hawa ni ahlul baytii* (watu wa nyumba yangu)".

Hadith hii utaipata katika uk. 146 wa Jz. 3 ya *al-Mustadrak alaa al-Swahiihayn* ya al-Hakim.

2 Tiz. Hapa chini sehemu ya 'Wake wa Mtume (s.a.w.w.) hawamo!'.

Hata hivyo, baada ya kuinukuu Hadith hiyo, Imam al-Hakim ameandika: "Hii ni Hadith sahihi kwa sharti za Bukhari, lakini hakuitoa (katika kitabu chake)."

2. Katika Uk. 116 wa Jz. 4 ya *Sahih Muslim* (kwa Kiingereza ni Hadith Na. 5955, uk. 1393-34, Jz. 4) imeandikwa kuwa: "Aisha amesema: 'Siku moja Mtume (s.a.w.w.) alitoka amevaa shuka iliyodariziwa kwa manyoya meusi. Akaja Hasan b. Alii; akamfinika. Kisha akaja Husein; akaingia pamoja naye. Kisha akaja Fatima; akamtia ndani. Kisha akaja Ali; akamtiandani. Kisha akasema: *Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaodolea nyinyi uchafu ahlul bayt*, *na kuwatakasa kabisa kabisa.*"

Hapa, kwa masimulizi yao wenyewe – wake wawili hao wa Mtume (s.a.w.w.) – tunaona kwamba Bwana Mtume (s.a.w.w.) **hakuwajumuisha** na kina Alii (a.s.), Fatima (a.s.) na watoto wao. Kwa hivyo – kwa kitendo chake hicho cha *kutowafinika* shuka yake hiyo – **ni wazi kwamba Bwana Mtume (s.a.w.w.) hakuwahisabu wake zake kuwa ni 'ahlul bayt' wake waliokusudiwa kwa aya tunayoizungumzia (Sura 33:33).**

Yasitoshe hayo! Bali hata mmoja wao (naye ni Bibi Ummu Salamah) alipotaka kuingia chini ya shuka hiyo, **Bwana Mtume (s.a.w.w.) hakumkubalia!** Kwa mfano, katika uk. 323 wa Jz. 6 ya *Musnad Ahmad* imeandikwa kwamba Ummu Salamah alisema: "Nikaiinua ile shuka ili niingie pamoja nao, Mtume (s.a.w.w.) **akanibwakura** na kusema: 'Wewe u katikka kheri'." Bali katika riwaya nyengine iliyomo uk. 198 wa Jz. 5 ya *Durrul manthur*, kuonesha kwamba neno *ahlul bayt* katika aya hii halina maana ya "wake wa Mtume." Ummu Salamah aliambiwa: "Wewe u katika kheri. Wewe u katika wake wa Mtume (*min azwaajin nabii*)."

Suali muhimu hapa zinazofaa tujiulize ni; Kama neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 limekusudiwa "wake wa Mtume (s.a.w.w.)", **kwa nini Mtume (s.a.w.w.) hakumruhusu Bibi Ummu Salamah kuingia chini ya shuka hiyo? Kwa nini alimwakura alipotaka kuingia? Kwa nini**

alimtumilia neno *az-waaj* na kumkatalia neno *ahlul bayt*? Kwa nini Bibi Aisha alipoona ameachwa nje, hakutaradhia naye kufinikwa?

Hujja nyengine – na hili ni muhimu sana ulitie maanani, ndugu msomaji – kinyume cha Hadith sahihi k.w.k zilizosema kuwa muradi wa neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 ni hawa watu watano tuliowashikilia sisi, **hakuna Hadith hata moja iliyo sahihi** – inayosema kuwa muradi wa neno *ahlul bayt* katika Sura hii ya 33:33 ni "wake wa Mtume (s.a.w.w.)."

HADITH TULIZOZITEGEMEA SISI

Mbali ya Hadith nyingi sana zilizomo katika vitabu vyetu (mashia) vya Hadith, ambazo nina hakika itamwiia vigumu Sheikh Mazuri kuzikubali kwa ajili ya msimamo wake, na wa madhihabi yake, ulivyo dhidi ya mashia na maimamu wao – kwa hivyo sikuzinukuu humu – hapa chini ninamnukulia zile zilizomo katika vitabu vya masunni ambao shekhe wetu huyo amejaribu sana katika kitabu chake tunachokijibu, na maandishi yake mengine dhidi yetu na imani zetu, kujikurubisha nao na kutaka aonekane ni wenzake! Lakini hata hizo zilizomo katika vitabu vya masunni, sitazinukuu zote kwa kuchela kukirefusha kitabu hiki. Nimeteuwa chahe tu kama sampuli. Nyengine, kwa wale wanaojua Kiswahili na wanaojua Kiarabu, nimewanukulia majina ya vitabu watakamoweza kuzipta Hadith hizo. Na hata vitabu hivyo sikuvitaja vyote. Nimevitaja vile vilivyozowewa kusomwa madarasani na miskitini mwetu huku Afrika ya Mashariki.

Sampuli Chache

Mbali ya zile riwaya mbili za wake wa Mtume (s.a.w.w.) tulizokwisha kuziona humu (uk. 3), riwaya nyengine ni kama zifuatazo:

1. Imepokewa kwa Abuu Said al-Khudrii kwamba amesema: "Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): 'Aya hii ilishuka kwa watu watano: kwangu, kwa Alii, kwa Fatima, kwa Hassan, kwa Husein: *Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea nyinyi uchafu ahlul bayt na kuwatakasa kabisa kabisa*'."

2. Imepokewa kwa Waathila b. al-Aqsa' (r.a.) akisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alikuja kwa Fatima akiwa na Hasan na Husein na Alii mpaka akaingia ndani. Akamsongeza Alii na Fatima; akawaketisha mbele yake. Akawaketisha Hasan na Husein, kila mmoja wao juu ya paja lake. Kisha *akawafinika kwa nguo yake*, na mimi nikiwa nyuma yao. Kisha akaisoma aya hii: *Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea nyinyi uchafu ahlul bayt na kuwatakasa kabisa kabisa*."

3. Imepokewa kwa Anas kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akipitia nyumba ya Fatima miezi sita, kila alipokuwa akitoka kwenda kuswali, na akisema: *"Swalaa! (enyi) ahlul bayt! Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea nyinyi uchafu ahlul bayt na kuwatakasa kabisa kabisa*."

4. Imepokewa kwa Ibn Abbas (r.a.) akisema: "Tumemshuhudia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) miezi tisa, kila siku anakuja kwenye mlango wa Alii b. Abii Twalib (r.a.) *wakati wa kila swala*, akisema: '*Assalaamu alaykum wa rahmatullaahi wa barakaatuhuu ahlal bayt*. *Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea nyinyi ucahfu ahlul bayt na kuwatakasa kabisa kabisa Swalaa! Mwenyezi Mungu awarehemu*.' Kila siku mara tano."

5. Imepokewa kwa Sa'd aliyesema: "Uliteremka wahyi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), akamwingiza Alii na Fatima na watoto wao wawili chini ya nguo yake. Kisha akasema: 'Hawa ni *ahlii* (watu wangu) na *ahlu baytii* (watu wa nyumba yangu).'"

Kama nilivyodokeza hapo juu, hizo ni sampuli chache tu ya Hadith nyingi sana zilizonukuliwa katika vitabu vingi sana na mashuhuri vya wanvyoni **wasio mashia** vya Hadith za Mtume (s.a.w.w.) na vya tafsiri ya Qur'ani, kutoka kwa maswahaba wakubwa wakubwa, na kukubaliwa na wanavyoni wakubwa wakubwa wa Hadith – **wasio mashia vile vile** – *kuwa ni sahihi*.

Maswahaba

Miongoni mwa maswahaba ambao zimepokewa kwao Hadith hizo ni hawa wafuatao:

1. Bibi Aisha bt. Abubakar, mke wa Mtume (s.a.w.w.)
2. Bibi Ummu Salamah, mke mwengine wa Mtume (s.a.w.w.)
3. Abdallah b. Abbas
4. Sa'd b. Abii Waqqas
5. Abuu Hureira ad-Duusi
6. Anas b. Maalik

7. Waathila b. al-Aqsa'
8. Abul Hamraa, yaani Hilal b. al-Harith
9. Abuu Said al-Khudrii
10. Jabir b.Abdillah al Answaarii
11. Umar b. Abii Salama
12. Thawbaan *mawlaa Rasulilah (s.a.w.w.)*

Maimamu wa Wapokezi wa Hadith

Miongoni mwa maimamu waliozipokea na kuzisimulia Hadith hizi ni:

1. Ahmad b. Hanbal (aliyefariki mwaka 241 H)
2. Abd b. Hamid al-Kish-shii (aliyefariki mwaka 249 H)
3. Muslim b. al-Hajjaaj, wa *Sahih Muslim* (aliyefariki mwaka 261 H)
4. Abuu Hatim Muhammad b. Idris al-Razi (aliyefariki mwaka 277 H)
5. Ahmad b. Abdil Khaaliq al-Bazzaar (aliyefariki mwaka 292 H)
6. Muhammad b. Isa al-Tirmidhii (aliyefariki mwaka 297 H)
7. Ahmad b. Shuayb al-Nasaaii (aliyefariki mwaka 303 H)
8. Abuu Abdillah Muhammad b. Alii al-Hakim al-Tirmidhii
9. Abuu Ja'far Muhammad b. Jarir al-Twabarii (aliyefariki mwaka 310 H)
10. Abdulrahman b. Muhammad b. Idris al-Razi, maarufu kwa jina la *Ibn Abii Hatim* (aliyefariki mwaka 327 H)
11. Sulayman b. Ahmad al-Twabaranii (aliyefariki mwaka 360 H)
12. Abuu Abdillah al-Hakim al-Niisaburii (aliyefariki mwaka 405 H)
13. Abuu Na'im Ahmad b. Abdillahi al-Asfahanii (aliyefariki mwaka 430 H)
14. Abubakr Ahmad b. al-Husayn al-Bayhaqii (aliyefariki mwaka 458 H)
15. Abubakr Ahmad b. Alii, maarufu kwa jina la *al-Khatib al-Baghdadii* (aliyefariki mwaka 463 H)
16. Abuu al-Sa'adat al-Mubarak b. Muhammad, maarufu kwa jina la *Ibn Amir* (aliyefariki mwaka 606 H)
17. Shamsuddil Muhammad b. Ahmad al-Dhahabii (aliyefariki mwaka 747 H)

18. Jalaluddin Abdulrahman b. Abubakar al-Suyutwii (aliyefariki mwaka 911 H)

Vitabu vya Hadith

Kama nilivyodokeza kabla, vitabu vya Hadith na Seera vilivyonukuu Hadith zisemazo kuwa *ahlul bayt* ni hawa watu watano tunaowashikilia sisi, ni vingi sana. Hata hivyo, hapa chini sivitaji vyote bali ninavitaja vile ambavyo vimezowewa sana huku kwetu Afrika ya Mashariki; nayo ni;

1. *Sahih Muslim*
2. *Sunanan al-Tirmidhii*
3. *Musnad Ahmad*
4. *Al-Mustadrak alaa al-Sahihayn*
5. *Talkhis al-Mustradak* ya al-Dhahabii
6. *al-Mu'jam al-Swaghir* ya al-Twabarani
7. *Usudul Ghaabah*
8. *Dhakhairul uqbaa* ya al-Twabari
9. *Maswabihus Sunnah* ya al-Baghawi
10. *Mishkaatul Maswaabiih* ya al-Umari
11. *al-Iswaabah* ya Ibn Hajar
12. *Muntakhab Kanzil Ummaal* iliyo pembezoni mwa *Musnad Ahmad*
13. *Fadhwaailul Khamsah*
14. *Al-Istiiab* ya Ibn Abdilbar iliyo pembezoni mwa *al-Iswaabah* (Na. 11 hapo juu)
15. *Yanaabiul Mawaddah* ya al-Qanduuzi

Vitabu vya Tafsiri ya Qur'ani

Kwa kutegemea Hadith zilizosimuliwa katika baadhi ya vitabu tulivyovitaja hapo juu na vyenginevyo, wanavyuoni wakubwa wakubwa wa Tafsiri ya Qur'ani – **wala hao si mashia!** – wamedokeza katika tafsiri zao kuwa waliokusudiwa kwa neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 ni hao watu watano: Mtume (s.a.w.w.), Alii (a.s.), Bibi Fatima na watoto wao wawili (a.s.). Hayo utayapata katika maelezo ya aya hiyo katika tafsiri zao hizo, kama vile:

1. *Tafsir Qurtubii*
2. *Tafsir al-Twabarii*
3. *Durrul Manthur* ya Suyuutwii
4. *Al-Kash-shaaf* ya Zamakhsharii
5. *Tafsir Ibn Kathir*
6. *Fat-hul Qadir* ya Shakwani
7. *Tafsirul Khazin*
8. *Tafsir Fakhrur Razi*
9. *Fat-hul Bayan* ya Siddiq Hassan Khan
10. *Asbaabun Nuzuul* ya al-Waahidii
11. *Ahkaamul Qur'an* ya al-Jas-Swaasw
12. *Shawaahidut Tanziil* ya al-Haskaani
13. *Ahkaamul Qur'an* ya Ibn Arabi

Alhamdulillah ndugu zetu wa *Al-Itrah Foundation* ya Dar es Salaam (S.L.P. 19701, na tavuti: www.alitrah.org) wameyafasiri kwa Kiswahili baadhi ya yaliomo katika baadhi ya vitabu hivyo na kuyachapisha kuwa jina la *Ahlul Bayt Ndani ya Tafsiri za Kisunni*. Jumla ni vitabu vitatu walivyoviita Sehemu ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu.

TUNAVYOJIFUNZA

Kwa kuzisoma Hadith hizo kwa mazingatio tunajifunza yanayofuata:

KWANZA: Kuwa muradi wa neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 ni Mtume (s.a.w.w.), Alii (a.s.), Bibi Fatima (a.s.), Hasan (a.s.) na Hussein (a.s.). *Hakuingia yoyote mwengine; si wake zake wala wanawake wowote wengine*.

Wake zake hawamo kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) **hakumruhusu yoyote kati ya wake zake** kuingia chini ya nguo waliyojifinika wao watano.

Wanawake wengine nao pia hawamo kwa sababu Mtume (s.a.w.w.), alipomtaka Bibi Fatima aje na mumewe na watoto wao wawili, *hakumtajia wengine wowote*: **hata wa ukoo wake mwenyewe (Mtume)!!**

Pili: Kuwa aya hiyo ya Sura 33:33 iliteremshwa *mbali* (peke yake) *kuhusu jambo maalumu*, kama tulivyokwisha kueleza humu. Bwana Mtume (s.a.w.w.) aliiweka hapo, katikati ya aya zinazozungumzia wake zake, *kwa lengo* maalumu ambalo pia tumelidokeza (uk. 17-18 humu). Lau waiondoa aya hiyo pale ilipo, utaona kwamba mtiririko wa aya za kabla yake (Sura 33:29-32 na sehemu ya kwanza ya aya ya 33) na za baada yake (Sura 33:34) zinazozungumzia wake zake, *hauathiriki hata chembe*!

Sheikh Mazrui Hakubali!

Lakini Sheikh Juma Mohammad Al-Mazrui, katika kitabu chake *Al-Qistasu Al-Mustaqim* (Mezani ya Haki), hakubaliani na sisi. Yeye anadai kwamba muradi wa neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 **sio** hawa watano tunaoshikilia sisi **bali ni wake wa Mtume (s.a.w.w.)**. Ameliteteta dai lake hilo kwa:

1. Hujja ya *sibaaq* na *siyaaq* (uk. 46-50)
2. Kanuni za kiuusli (uk. 50-60)
3. Hujja ya kilugha (uk. 62-65)
4. Kuzijeruhi *sanad* za Hadith *kumi* (uk. 76-111) kati ya zile *nyingi* tunazozitolea ushahidi sisi

Hizo inshallah tunazijibu humu katika sura inayofuatia. Lakini, hata hivyo, la kushangaza kabisa ni kwamba, ijapokuwa sisi hutoa Hadith za kutilia nguvu dai letu kuwa *ahlul bayt* ni hao watano, Sheikh Mazrui **hakujasiri hata mahali pamoja** katika kitabu chake kututajia ile Hadith mashuhuri itumiwayo kutilia nguvu dai lake la kuwa "ni wake wa Mtume". Hata hivyo, sisi tunainukuu humu Hadith hiyo na kutoa sababu zetu za kuikatalia (uk. 33-36) ambapo twataraji itakudhihirikia, ndugu msomaji, kwa nini shekhe wetu huyo hakusubutu kuitaja kama hujja yake ya kudaiya dai lake!

HUJJA ZAKE

Katika kuikataa tafsiri tuliyotegemea sisi, ya neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33, Sheikh Mazrui ametoa hujja zake na maelezo yake kuanzia uk. 46 wa kitabu chake. Hata hivyo hakuwa na kauli moja; zake ni kauli mbili: mara *ahlul bayt* **ni** wake wa Mtume (s.a.w.w.) (tiz. Uk. 58, 61, 67, 72, 75, 174 n.k. wa kitabu chake); mara wao **ni katika** *ahlul bayt* (tiz. uk. 44, 113 n.k.). Lakini kwake yeye kama mfuasi wa madhihabi yake ya Ibadhi; na kwa sababu za kihistoria zinazoeleweka - mategemeo yake makubwa ni yale ya kuwa "*ahlul bayt* **ni** wake wa Mtume (s.a.w.w.)", kama inavyomdhihirikia msomaji yoyote anayekisoma kitabu chake kwa utafiti na mazingatio.

Kulitetea hilo, shekhe wetu huyo, kwa "utaalamu" mkubwa, ametegemea hujja nne tulizozitaja humu (uk. 14) na kusema kwamba hayo ni "miongoni mwa mambo ambayo wanavyuoni wa tafsiri wanayazingatia katika kuifasiri Qur'ani." (tiz. uk. 46 wa kitabu chake.)

Hata hivyo, la kushangaza hapa ni kwamba shekhe wetu huyo *hakupenda*, au labda *ameghafilika*, kutaja kuwa: jinsi Mtume (s.a.w.w.), alivyofasiri au alivyoifafanua aya fulani **ndilo jambo la kwanza kubwa na lililo muhimu kuliko yote** ambalo wanavyuoni wa tafsiri hulizingatia katika kuifasiri Qur'ani. Vipi wataacha kulizingatia hilo na lhali yeye (s.a.w.w.) ndiye aliyepewa jukumu la kwanza (Sura 16:44) la kutufasiria na kutufafanulia aliyoteremshiwa na Mola wake? Isitoshe! Tukaambiwa kwamba anayotupa yeye tuyachukue (Sura 59:7) kwa sababu hasemi analosema kwa hawaa ya nafsi yake ila huwa ni wahyi aliofunuliwa (Sura 53:3-4). Basi mambo yakiwa ni hivyo, ni mwanachuoni gani wa tafsiri, aliye mwislamu, atakayethubutu kuikosoa tafsiri ya Mtume (s.a.w.w.) **kwa sababu tu** haiowani na "msingi" ya tafsiri walivyojiwekea wao (wanavyoni)?! Na kweli wako wanavyoni wa aina hiyo? Hebu tuwasome wawili watatu **ambao kamwe si mashia** *bali hata wakati mwengine huwapinga khaswa*! Hao ni:

1. Ibn Taymiyya ambaye upinzani wake dhidi ya mashia na maimamu wao u maarufu sana. Yeye – katika uk. 18, Jz. 13 – wa kitabu chake kilichokusanya fatwa zake kiitwacho *Majmuu'atul Fatawaa*, amesema: "Na katika yanayohitajia kujulikana ni kwamba: Qur'ani na Hadith, ikijulikana tafsiri yake kutokamana na Mtume (s.a.w.w.), *haitahitajia maneno ya wana-lugha (ahlul lughah) kwa hilo kwa sababu tafsiri yake ishajulikana. Na lililokusudiwa kwa hilo kutokamana na Mtume (s.a.w.w.) halitahitajia kutolewa ushahidi kwa maneno ya wana-lugha wala wengineo*."

2. Muhammad Naisruddin al-Albani ambaye ni maarufu sana kwa mashekhe vijana huku kwetu kuwa ni "Bukhari wa zama zetu." Yeye katika kitabu chake kidogo alichokiita *Manzilatus Sunnah fil Islami Wa Bayaanu Annahuu Laa Yustaghnaa 'Anhaa bil Qur'an*, na chini ya kipambanuzi (*fasl*) alichokiita *'Adamu Kifaayatil Lughati Lifahmil Qur'an* (maana yake: Kutotosheka kwa lugha kuifahamia Qur'an) amesema: "Na kutokana na yaliyotangulia inadhihiri wazi kwamba hapana nafasi kwa yoyote – awe mjuzi atakavyokuwa wa lugha ya Kiarabu na aya zake – kuifahamu Qur'ani tukufu *bila ya kutafuta msaada wa Sunnah za Mtume (s.a.w.w.)* - za maneno (*qawliyyah*) na za vitendo (*fi'liyyah*) – *maana yeye hatakuwa ni mjuzi wa dini kushinda maswahaba wa Mtume (s.a.w.w.) ambao Qur'ani ilishuka kwa lugha yao...*"

3. Al-Imam Abii Muhammad al-Hasan b. Alii b. Khalf al-Barbahaari. Yeye, katika uk. 119 wa kitabu chake kiitwacho *Sharhus Sunnah* amesema hivi: "Ukimsikia mtu unapomtolea *athar* (Hadith) *yeye haitaki (bali) anaitaka Qur'ani (tu)*, basi usiwe na shaka kwamba mtu huyo yuna uzandiki...Basi mwinukie na umwache."

Kwa madondoo hayo mawili matatu, itakudhihirikia ndugu msomaji, kwamba kabla ya kukimbilia *sibaaq* na *siyaaq* ya aya, kanuni za kiusuli na kilugha n.k. – kama alivyofanya Sheikh Mazrui - mahali pa kwanza pa kukimbilia ni kwenye *sunnah* za Mtume (s.a.w.w.).

Inapokuwa hakuna *sunnah* za Mtume (s.a.w.w.) **ndipo hapo** tukimbilie *sibaaq* na *siyaaq*, aya nyengine za Qur'ani n.k.

Sasa, baada ya kulisema hilo kwa mukhtasari, na kulitolea ushahidi, hebu tuzitathmni zile hujja nne alizozitoa Sheikh Mazuri kuwa ni "miongoni mwa mambo ambayo wanavyoni wa tafsiri wanayazingatia katika kuifasiri Qur'ani."

Sibaaq na Siyaaq

Sibaaq ni maneno yaliyotangulia, na *Siyaaq* ni maneno yanayofuatia. Kwa mujibu wa Sheikh Mazrui, **ili** tuweze kuelewa kwa nini neno *ahlul bayt* – lililomo katika Sura 33:33 - liwe na maana ya "wake wa Mtume (s.a.w.w.)" ni lazima tuangalie aya hiyo imetanguliwa na maneno gani na imefuatiwa na maneno gani. Kwa kuwa maneno yaliyoitangulia aya hiyo ni yale ya Sura 33:29 mpaka yale ya sehemu ya kwanza ya Sura 33:33 – ambayo ndiyo *sibaaq* – na yale ya Sura 33:34 – ambayo ndiyo *siyaaq* – yanazungumzia "wake wa Mtume (s.a.w.w.)", ni lazima hapo – kwa mantiki ya Sheikh Mazrui - neno *ahlul bayt* katika sehemu ya pili ya Sura 33:33 liwe na maana ya "wake wa Mtume (s.a.w)!".

Majibu Yetu:

Sisi hatuikubali tafsiri au mantiki ya Shekhe wetu huyo kwa sababu zifuatazo:

i. Inapingana na tafsiri ya Bwana Mtume (s.a.w.w.) kama ilivyo katika Hadith zake kadhaa wa kadhaa zilizokubaliwa kuwa ni sahihi, si na wanavyoni wa Kishia peke yao bali hata wa Kisunni (tiz. uk. 8 humu). Kwa kuwa tafsiri aliyotuachia Bwana Mtume ni hii tuliyoishikilia sisi, hatuwezi kuiacha na kuishika ya wengine – wawe wawao- maana kufanya hivyo itakuwa ni kwenda kinyume na amri ya Mwenyezi Mungu iliyomo katika Sura 59:7.

ii. Ukiichunguza Qur'ani kwa makini utaona kwamba aya zake hazikupangika kwa mtiririko wa kihistoria. Kwa mfano, utaona kwamba baadhi ya sura za *Madaniyya* (zenye aya zilizoteremshwa **baada** ya Mtume kuhamia Madina) ziko **mbele** ya baadhi ya zile

za *Makkiyya* (zilizoteremshwa pale Mtume **bado yuko** Makka)! Au, katika sura nyengine, utaona aya zilizoteremshwa Makka **zimechanganywa pamoja na** zile zilizoteremshwa Madina **katika sura moja**: ya *Makkiyya* au *Madaniyya*! Kwa nini ikawa hivyo? Sababu iliyo wazi ni kwamba hivyo ndivyo Bwana Mtume (s.a.w.w.) alivyozipanga aya hizo na sura hizo **kwa hikima aliyolekezwa na Mola wake.**

Ukilielewa hilo ndipo utakapoweza kuelewa kwa nini maneno "Hakika Mwenyezi Mugu anataka kuwaondolea uchafu...kabisa kabisa"- **ambayo ni aya mbali**, kinyume na alivyoelewa Sheikh Mazrui kuwa ni moja (tiz. uk. 49 wa kitabu chake) – yamewekwa pamoja na maneno: "Na kaeni majumbani mwenu...na mtwiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake" katika hiyo hiyo Sura 33:33.

Ni aya mbali kwa ushahidi gani? Kwa ushahidi wa Hadith iliyopokewa kwa Bibi Ummu Salamah (uk. 3 humu) mke wa Bwana Mtume (s.a.w.w.), kuwa kipande cha pili cha aya hiyo kiliteremshwa nyumbani kwake. Katika Hadith hiyo Bibi Ummu Salamah **hakukitaja hicho kipande cha kwanza cha aya hiyo.**

Jee, Mtume (s.a.w.w.) ameiweka hapo kwa hikima gani? Ameiweka hapo kwa hikima tuliyoieleza humu katika uk. 17. Tafadhali itizame.

iii. Kuwa neno *ahlul bayt* lina maana ya "wake wa Mtume (s.a.w.w.)" **kwa sababu tu** limekuja baina ya aya zinazozungumzia wake zake hao si hujja! Kwa nini? Kwa sababu tunaona, tunapoisoma Qur'ani, kwamba si lazima iwe hivyo. Hebu tutosheke na hii mifano miwili tu kwa sasa:
   a. Ule wa Sura 5:3 usemao: "Mmeharimishiwa nyamafu wa damu na nyama ya nguruwe, na kilichochinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kilichokufa kwa kusongeka koo, na kilichokufa kwa kupigwa na kilichokufa kwa kuanguka, na kilichokufa kwa kupigwa pembe (na mwengine) na kilicholiwa na mnyama (kikafa) ila mkiwahi hukichinja kabla hakijafa. Na

(pia mmeharimishiwa) kilichochinjwa panapofanyiwa ibada isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu. Na (ni haramu kwenu) kutaka kujua siri kwa kuagua kwa mabao. Hayo yote ni maasi. Leo waliokufuru wamekata tamaa na dini yenu. Basi msiwaogope, bali niogopeni mimi. **Leo nimewakamilishia nyinyi dini yenu, na kuwatimizia neema Yangu, na kuwapendelea Uislamu uwe dini yenu.** Na mwenye kudharurika kwa njaa, pasi na kulekea kwenye dhambi (akala hivi vilivyoharimishwa), hakika Mwenyezi Mungi ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu".

b. Ule wa Sura 12:28-29 usemao: "Basi (mumewe) alipoona kanzu yake imechanwa kwa nyuma, alisema: Hakika hii ni katika vitimbi vyenu (nyie wanawake); kwa hakika vitimbi vyenu ni vikubwa. **Yusuf! Yaachilie mbali haya.** Na wewe (mwanamke) omba msamaha kwa dhambi zako. Hakika wewe ni katika wafanyao makosa."

Katika mifano miwili ya aya za Qur'ani tuliyoitoa hapo juu - mbali ya mengine tuliyoiacha – utaona kwamba maneno tuliyoyachapa **kwa wino mzito** si sehemu ya maneno yaliyotangulia wala ya yale yaliyofuatia. Ukiutizama mfano (a) utaona kwamba, katikati ya vifungu vinavyozungumzia vilivyoharimishwa kuliwa, mna kifungu kinachozungumzia kukamilishwa dini (tulichokichapa **kwa wino mzito**). Sasa *kimaudhui*, vinahusiana vipi vifungu viwili hivyo? Hali kadhaalika ukiutizama mfano (b), utaona kwamba maneno aliyoambiwa Nabii Yusuf (tuliyoyachapa **kwa wino mzito**) hayana mtirirko mmoja na yale yaliyoyazunguka ya kumkemea yule mke wa waziri aliyemsingizia Nabii Yusuf kuwa alimtaka bila ya yeye (yule mwanamke) kumtaka (Sura 12:26).

Ili hili tunalosema likufunukie zaidi, hebu jaribu kuzisoma – au ziandike kisha uzisome - aya za mifano yote mwili bila ya hayo maneno tuliyoyachapa **kwa wino mzito**. Jee, kuyaondoa maneno hayo *kumeathiri kwa vyovyote vile* ule mtirriko wa maneno yaliyo baina yake? Bila shaka hayakuathiri! Basi vivyo hivyo ndivyo maneno ya

“Hakika Mwenyezi Mungu anataka... kuwatwaharisha kabisa kabisa” (Sura 33:33) – yaliyo baina ya Sura 33:28 na Sura 33:34 – yalivyo. Lau utayaondoa hapo, na usome maneno yaliyobakia kuanzia Sura 33:28 hadi Sura 33:34 – bila ya kifungu hicho – utaona kwamba mtiririko wake, wa kuwakhatibu wake wa Mtume (s.a.w.w.), haukauthirika kwa namna yoyote ile.

Mtindo wa kuweka kifungu cha maneno aina hiyo, katikati ya vifungu vyengine vya maneno visivyoowana nacho, huitwa ***istidraak*** (*Digression*) katika balagha ya lugha; nayo hutumiuwa mara kwa mara na wazungumzaji na waandishi wa Kiarabu na wengineo.

Lakini hapa *kwa nini Bwana Mtume (s.a.w.w.) akayaweka maneno hayo katikati ya aya zinazowakhatibu wake zake*? Hilo tutalielewa vyema tukianzia Sura 33:**28** – sio Sura 33:**29** kama alivyofanya Sheikh Mazrui (uk. 49 wa kitabu chake) – ambapo Mwenyezi Mungu anamwamrisha Mtume wake awakhtarishe wake zake aina ya maisha wanayopenda kuyaishi. Kama watapenda maisha ya hii dunia na mapambo yake, basi yeye Mtume (s.a.w.w.) hatayaweza hayo. Kwa hivyo bora waje, awape kitoka-nyumba chao na awaache kwa wema. Lakini (Sura 33:29 sasa) kama wanamtaka Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na nyumba ya Akhera, basi atakaa nao pamoja na kuwahakikishia kuwa Mwenyezi Mungu atawalipa malipo mema. Hata hivyo wajue kwamba (Sura 33:30 sasa) yoyote katika wao atakayefanya maovu ataadhibiwa kawili (*double*). Hali kadhaalika (Sura 33:31 sasa), yoyote katika wao, atakapomtwii Mwenyezi Mungu atampa malipo yake mara mbili na kumwandalia riziki yenye hishima.

Lakini kwa nini kuambiwa kwamba watafanyiwa yote hayo, *tafauti na wake wa watu wengine*? Sababu kubwa ni kuwa wao (Sura 33:32 sasa) “**Si kama yoyote katika wanawake wengine**” (lakini) *iwapo watamcha Mwenyezi Mungu*. Wakakumbushwa pia kwamba wasizilegeze sauti zao wanapozungumza na watu, na (*sehemu ya kwanza* ya Sura 33:33 sasa) wakae majumbani mwao, wala wasioneshe mapambo yao kama wanawake wa zama za Ujahili walivyokifanya, wasimamishe swala,

watoe zaka, wamtwii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na (Sura 33:34 sasa) wayataje yale yasomwayo majumbani mwao ya aya za Mwenyezi Mungu na hikima zake.

Baada ya kuyasoma yote haya na kuyazingatia, tuna haki ya kujiuliza: kwa nini yakadondolewa yote hayo na mengine ambayo hawakuwekewa wake wa watu wengine? Majibu yake tutayapata kwanza katika aya ya 32 isemayo kwamba: wao; wake wa Mtume (s.a.w) "**si kama yoyote katika wanawake wengine**." Wao wameolewa katika "Nyumba" ya mtu mtukufu ambaye Mwenyezi Mungu anataka kuiondolea uchafu na kuitakasa kabisa kabisa (Sura 33:33).

Kwa hivyo lazima wachunge miondoko yao - kwa kufuata yote yaliyodondolewa kuanzia Sura 33:28 hadi Sura 33:34 – wasije wakaileteа aibu na kashfa Nyumba ya Mtume (s.a.w.w.). Ndipo Mtume (s.a.w.w.) **akakiweka** hicho *kipande cha pili* cha Sura 33:33 katikati ya Sura 32:38 na Sura 33:34. Hili tutalielewa vizuri zaidi tunapomwambia mwanamke aliyeolewa katika "nyumba" yenye hishima: "Ewe mke wa fulani! Wewe si kama wake wa watu wengine. Wako wewe ni mume anayetokana na nyumba ya watakatifu ambao Mwenyezi Mungu amewahifadhi na machafu na kuwakinga na mapungufu. Kwa hivyo jisitiri na jiwekee hishima."

Katika fuo (*context*) la maneno kama hayo – na ndivyo ya khaswa ilivyo katika Sura 33:33 – neno *nyumba* hapo halina maana ya "nyumba yoyote ya udongo au mawe". Ina maana ya nyumba maalumu.

iv. Ukiziangalia aya zilizokhatibiwa wake wa Mtume (s.a.w.w.) – kuanzia Sura 33:28 hadi 33:34 – utaona kwamba Mwenyezi Mungu amewakhatibu kwa dhamiri ya kike ya lugha ya Kiarabu: inkuntu**nna**, turid**na**, fata'aala**yna**, lastu**nna**, inittaqaytu**nna**, takhdwa'**na**, qul**na**, waqar**na**, biyutiku**nna**, tabarraj**na**, aqim**na**, aat**iina**, atwi'**na**, wadhkur**na**. Hiyo, kwa mujibu wa kanuni za nahau (sarufi) ya Kiarabu, hutumiliwa wanawake *wanapokuwa ni wao peke yao*; hamna mwanamume. Lakini tukija kwenye Sura

33:33 yenye neno *ahlul bayt*, tunamwona Mwenyezi Mungu hakusema *liyudh-hiba ʻanku***nna** *al-rijsa wala wayutwahhiraku***nna** (kwa dhamiri ya kike) bali *liyudh-hiba ʻan***kum** *al-rijsa* na *wayutwahhira***kum** (kwa dhamiri ya wanaume peke yao, au wanapokuwa na wanawake japo mmoja). Kwa hujja hii, kwa hivyo, haiwezekani kuwa neno *ahlul bayt* katika aya hii limekusudiwa "wake wa Mtume (s.a.w.w.)" – khaswa kwa vile ambavyo, baada ya kutumia dhamiri ya kiume kama tulivyoona hapo juu, Mwenyezi Mungu alirudia dhamiri ya kike katika aya inayofuatia ya Sura 33:34; akasema *wadhkur***na** na *buyuutiku***nna**.

v. Zaidi ya hayo, siyo kwamba *wake wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.)* hawakutajwa katika Qur'ani Tukufu; la! Wametajwa, lakini si kwa jina la *ahlul bayt*! Mara sabaa wametajwa kwa jina la *az-waaj* (tiz. Sura 33:6, 28, 50, 53, 59 na Sura 66:1 na 3). Na mara mbili kwa jina la *nisaa an-nabiy* (tiz Sura 33:30 na 32). Basi kwa nini, na katika aya hii tunavyoijadili, wasitajwe kwa jina mojalo ya hayo mawili - **khaswa kwa hivi ambavyo**, baina ya aya ya 28 na 34 ya Sura *hii hii ya al-Ahzaab*, jina la *az-waaj* limetajwa mara moja (aya 28), na jina la *nisaa an-nabiy* limetajwa mara mbili (aya ya 30 na 32)? Hili ni kuonesha kwamba neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 halina maana ya "wake wa Mtume (s.a.w.w.)."

Kanuni za Kiusuli

Kuanzia uk. 50 mpaka uk. 61 wa kitabu chake, Sheikh Mazrui - akitufafanulia kanuni za kiusuli kama msingi mwengine wa kufasiria Qur'ani - ametunukulia aya kadhaa wa kadhaa zenye neno *inna* na neno *innamaa*, na kutueleza kwa mbwembwe na vishindo - kwa kutumia istilahi za kiusulli – matokeo ya matumizi hayo katika aya ambamo maneno hayo yamo.

Akatuelezea (katika uk. 50 wa kitabu chake): "Katika elimu ya *usulil-fiq-hi* kuna kitu kinaitwa "*illa*" nayo ni sababu iliyopelekea kuwepo kwa hukumu fulani au yenye kueleza kwa nini pametolewa hukumu fulani au kwa nini pamesemwa maneno fulani."

Kisha akaendela (katika huo huo uk. 50): "Sasa "*illa*" (sababu) ziko za namna mbili kuu. Moja katika aina mbili hizi ni "*al-ilali al-manswuswu alayhaa*" (sababu zilizoelezwa kwa uwazi). Hizi kuna njia zake za kuzijua. Miongoni mwa njia hizo ni pale panapotajwa amri, au katazo au - wakati mwengine – habari kisha ikatiliwa mkazo kwa kuletwa herufi "**INNA**" ambayo *hamza* yake (*Alifu* yake) ina *Kasra* na *Nuni* yake ina *Shada*, basi hii huwa imeeleza "*illa*" (sababu) ya amri hio au katazo hilo au habari hio iliotajwa kabla yake. Na hii ni pale ambapo kuna mfungamano wa maana baina ya maneno yaliyotangulia kabla ya herufi "**INNA**" na maneno yanayofatia baada yake."

Baada ya hapo akatoa mifano mitatu (uk. 50-51) ya *illa* (sababu) iliyoletwa na herufi *inna* **baada ya amri**, mifano miwili (uk. 52-53) iliyoletwa na herufi *inna* **baada ya katazo**, na mifano miwili mengine (uk. 53-54) iliyoletwa na herufi *inna* **baada ya habari**.

Ndipo mwisho akamaliza maelezo yake hayo kwa maneno haya ambayo ndiyo aliyoyapendela yeye (uk. 54-56):
"Kama umeyafahamu hayo niliokueleza, basi tayari utakuwa umefahamu uhusiano baina ya maneno ya sehemu ya kwanza ya Aya hiyo ya 33 ya Sura ya 33, na maneno ya sehemu ya pili ya Aya hio. Kwani maneno ya pili ni *ta'liilul limaa sabaqa minal kalaami* (yenye kueleza "*illa*" (sababu): kwa nini kumekuwa na maneno yaliotangualia), na herufi iliotumika kuonesha "*illa*" (sababu): ni herufi ile ile "**INNA**", jambo ambalo linaonesha kuwepo kwa mfungamano baina ya maneno ya kwanza yalio kabla ya herufi "**INNA**" na maneno yalio baada ya herufi hio. Na kwa hivyo wahubiriwa wa sehemu ya kwanza ndio wahubiriwa katika sehemu ya pili".

Kwa maelezo haya, Sheikh Mazrui kwa ufupi – na ndivyo khaswa alivyofanya kwa urefu (uk. 55-56) – anataka kutueleza kwamba kwa kuwa aya isemayo: "*Hakika (**innamaa**) Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu, enyi watu wa Nyumba ya Mtume, na kuwatakasa kabisa kabisa*" (ambayo ni aya ya 33) imewekwa **baada** ya aya ya 32 yenye mambo **waliyokatazwa** na **waliyoamrishwa** wake wa Mtume

(s.a.w.w.); na kwa kuwa **baada ya makatazo** hayo na **amri** hizo imefuata "*illa*" (sababu) ya kutolewa amri hizo na makatazo hayo – kutumiwa neno "**INNA**" – inatakikana tufahamu "kwamba kuna mfungamano wa lazima na wa nguvu" baina ya maneno ya aya ya 32 pamoja na yale ya sehemu ya kwanza ya aya ya 33, na yale ya sehemu ya pili ya aya ya 33, ambayo ndiyo tunayoyajadili, yaliyoanza kwa "Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu... na kuwatakasa kabisa kabisa." Tukifahamu hivyo ndipo itakapotuthubutikia "kwamba wahubiriwa (addresses) katika Aya ya 32 na sehemu ya kwanza ya Aya ya 33, ndio wahubiriwa katika sehemu ya pili ya Aya hio ya 33." Akamaliza kwa kujigama kwamba: "Hii ndio natija ya tafsiri inayopatikana katika Aya hio ikiwa tutakwenda na misingi na fani zinazotumika katika kuifasiri Qur'ani. Vyenginvyo itakuwa hatukwenda kifani, bali tunakwenda Kihashwiya (kuchukua juu juu tu), na huku tunawalamu wenzetu kwa jambo hilo hilo."

Kana kwamba *mufassirin* wote wakubwa wakubwa – *waarabu* na *wasio waarabu*, *mashia* na *wasio mashia* – hawakwenda na "misingi na fani zinazotumika katika kuifasiri Qur'ani" **kwa sababu tu** hawakuifasiri aya hiyo ya 33 kwa tafsiri aliyoishikilia yeye!! *Wote hao* "wamekwenda Kihashwiya"!! *Subhaanallah*!

Majibu Yetu:

Sisi hatuna mushkili na maelezo ya Sheikh Mazrui kuhusu umuhimu wa matumizi ya kanuni za kiusuli katika kufasiria Qur'ani. Wala hatupingi kwamba linapotumiwa neno *inna* au *innamaa* **baada ya** kutolewa **amri**, **katazo** au **habari** huwa limeeleza *illa* (sababu) ya *amri* hiyo, *katazo* hilo au *habari* hiyo. **Tusilolikubali sisi** ni hivi shekh wetu huyu alivyofungamanisha amri na makatazo yaliyomo katika aya ya 32 na ya sehemu ya kwanza ya aya ya 33 (tiz. uk. 56 wa kitabu chake) na *illa* (sababu) iliyomo katika sehemu ya pili ya aya ya 33. Kwa kufanya hivyo bila shaka atafikia uamuzi alioutoa. Lakini jee hivyo ndivyo sawa?

Majibu yetu ni: La! Sivyo! Pa kuanzia **si** pa aya ya 32 na sehemu ya kwanza ya aya ya 33, kama alivyofanya Sheikh Mazrui (tiz. uk. 55 wa kitabu chake).

Pa kuanzia **ni** aya ya 28. Hapo utaiona **amri** ambayo Mwenyezi Mungu alimpa Mtume wake kwa kumwambia: "Ewe Mtume! **Wambie** wake zako.."

Kisha ikaja aya ya 32. Humo, katika jumla ya mambo ambayo Mwenyezi Mungu **alimwamrisha** Mtume wake awambie wake zake, mna **katazo** na **amri** na **habari**. **Katazo** lenyewe ni wake wa Mtume *wasilegeze* sauti zao wanaposema na watu. **Amri** ni, wanaposema, *waseme maneno mazuri*. Na **habari** ni kwamba *wao si kama yoyote katika wanawake wengine – iwapo watamcha Mwenyezi Mungu*.

Baada ya hapo ndiyo ikaja aya ya 33 ambamo humo pia, katika sehemu yake ya kwanza, mna **amri** kadhaa na **katazo moja**. **Amri** zenyewe ni: "Kaeni majumbani mwenu, simamisheni swala, toeni zaka, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake"; na **katazo** lenyewe ni "*msidhihirishe mapambo yenu kama yaliyokuwa yakidhihirishwa katika jahilia ya kizamani*."

Baada ya *amri* hizo, *makatazo* hayo na *habari* hizo ndipo Mwenyezi Mungu alipotoa "*illa*" (sababu) ya yote hayo kwa kuianzia sehemu ya pili ya aya ya 33 kwa neno **innamaa**.

Kwa maelezo haya mafupi itatudhihirikia kwamba: kama tutaanzia **amri** ambayo Mwenyezi Mungu alimpa Mtume wake katika Sura 33:28, ikaandamiwa na **amri**, **makatazo** na **habari** zilizomo kuanzia Sura 33:29 hadi sehemu ya kwanza ya Sura 33:33 – ambazo Mtume (s.a.w.w.) aliwapa wake zake – ndipo tutakapoweza kuelewa vizuri kwa nini Mtume (s.a.w.w.) aliiweka hapo *sehemu ya pili* ya Sura 33:33 (ambayo ilishuka mbali) iliyoanza kwa neno **innamaa** kuonesha "*illa*" (sababu) ya amri hizo na makatazo hayo. Ukitaka kuijua sababu hiyo, isome tulipoitasua kwenye uk. 18 humu.

Hujja ya Kilugha

Mas-ala ya msingi tuliyonayo hapa ni: jee, neno *ahlul bayt*, lililo katika Sura 33:33 – ambalo ndilo tunalolijadili hapa – "**ni** sawa sawa" na

lile lililo katika Sura 11:73 isemayo: "*Wakasema (wale malaika): jee unastaajabia amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na baraka Zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii (***ahlul bayt***)!...?*"

Sheikh Mazrui anasema "**ni** sawa sawa" kwa hujja kwamba "kanuni kuu na ya msingi ya tafsiri ya Qur'ani ni kuifasiri Qur'ani kwa Qur'ani, kwani Qur'ani ni wahyi, na wahyi haugongani, na kwa hivyo katika Aya zake nyingi, Qur'ani huwa inajifasiri yenyewe kwa yenyewe." Kisha akauliza; "Vipi mke wa Nabii Ibrahim kawa miongoni mwa AHLUL-BAIT kwa mujibu wa andiko la wazi la Qur'ani na vipi wake wa Nabii Muhammad wasiwe katika AHLIL-BAIT?" (tiz uk. 65 wa kitabu chake).

MAJIBU YETU:

Sisi twasema "**si** sawa sawa" kwa hujja zifuatazo:

Kwanza: Ijapokuwa ni kweli kwamba Qur'ani yajifasiri yenyewe kwa yenyewe, **lakini si kweli** kwamba neno moja likija kwa maana moja katika aya moja, **lazima** likae kwa maana ile ile, au "sawa sawa", katika aya nyengine. Hebu tuangalie mifano miwili mitatu hapa chini:

a. Tuangalie neno *an-naas* (kwa wingi) lililokuja kama mara 240 hivi katika Qur'ani Tukufu. Kwa kawaida neno ili maana yake ni *watu*. Lakini katika mwanzo wa Sura 3:173 – isemayo: "*Ambao waliambiwa na* **watu***: Hakika* **watu** *wamewakusanyikia nyinyi; basi waogopeni!..*" – neno hilo, ambalo limekuja mara mbili katika hiyo hiyo aya moja, halikuja kwa maana moja au sawa. Wanavyotwambia wanavyoni wa tafsiri ni kwamba hiyo "watu" ya pili katika aya hiyo imekuja kwa maana yake ya kawaida, kilugha: ya watu wengi. lakini hiyo "watu" ya kwanza haikuja kwa maana hiyo, bali imekuja kwa maana ya **mtu mmoja tu** aliyekiitwa Nuaym b. Mas'uud. *Yeye* ndiye aliyewatisha *hao watu wengine.*[1]

b. Tuangalie neno *nisaa-anaa* (wanawake wetu) lililokuja mara zisizopungua 59 katika Qur'ani Tukufu. kwa kawaida neno *nisaa* (kwa wingi) maana yake ni *wanawake* au *wake*. Lakini katika

1 Hilo utalipata takriban katika Tafsir zote kubwa za Qur'ani.

Sura 3:61 – isemayo: "*Basi watakaokuhuji katika haya baada ya kukufikilia ujuzi huu, wambie: Njooni tuwete watoto wetu na watoto wenu, na* ***wanawake wetu*** *na* ***wanawake wenu****, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa uyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo*". – neno hilo ambalo, kama *an-naas* hapo juu, limekuja mara mbili katika hiyo hiyo aya moja, halikuja kwa maana moja au sawa. Wanavyotwambia wanavyoni wa tafsisi ni kwamba hiyo "wanawake" ya pili katika aya hiyo imekuja kwa maana yake ya kawaida, kilugha: ya wanawake au wake wengi. Lakini hiyo "wanawake" ya kwanza haikuja kwa maana hiyo, bali imekuja kwa maana ya **mwanamke mmoja tu**, naye ni Bibi Fatima, binti ya Mtume (s.a.w.w.).[2]

Na ijapokuwa iliposhuka aya hiyo Bwana Mtume (s.a.w.w.) alikuwa tayari anao wake zake, na ijapokuwa neno hilo limekuja kwa maana ya *wake wa Mtume* katika aya nyengine (k.v. Sura 33:30 na 32), lakini katika sura hiyo ya 3:61 halikuja kwa maana ya *wanawake* (kwa wingi) **wala** *wake wa watu fulani*, **wala hata** *wake wa Mtume (s.a.w.w.)*, **bali** kwa maana ya *mwanamke mmoja maalumu*; naye ni Bibi Fatima (a.s.).

Basi na vivyo hivyo ndivyo lilivyo neno *ahlul bayt*; **si lazima** muradi wake katika Sura 33:33 uwe "ni sawa sawa" na ule wa Sura 11:73 au Sura 28:12, au hata wa ile Hadith ya Bukhari aliyoitaja Sheikh Mazrui katika uk. 67 wa kitabu chake, au hata wa ile Hadith mashuhuri ya kuwa Salman al-Faarisi ni katika *ahlul bayt*.[3]

Pili: Kwa kuwa sisi na Sheikh Mazrui tunakhtalifiana kuhusu makusudio ya neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33, jee sisi, *kama waislamu*, inatakikana turejee kwa nani ili atuhukumie kesi yetu?

Kwa mujibu wa Qur'ani (Sura 4:59) inatakikana turejee kwa Mwenyezi Mungu (yaani kwa hiyo hiyo Qur'ani). Jee iwapo, hata baada ya

2 Hili pia ni kama Na. 1 hapo juu

3 Uk. 201 wa Jz. 6 wa *Tahdhib Tarikh Dimishq*

kuirejelea hiyo Qur'ani, bado tunazozana – kama hivi tulivyo sasa – turejee kwa nani mwengine? Kwenye aya hiyo hiyo tunaambiwa kwamba, iwapo ni hivyo, basi turejee kwa Bwana Mtume (s.a.w.w.). Kwa nini turejee kwa Bwana Mtume (s.a.w.w.)? Ni kwa sababu mbili kubwa:

a. Ni kwa sababu kwamba, **baada ya Mwenyezi Mungu**, *hakuna yoyote mwengine* anayeelewa maana ya maneno ya Qur'ani, na *muradi wake*, kumshinda Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Maana yeye ndiye *aliyeteremshiwa* hii Qur'ani na Mwenyezi Mungu, na yeye vile vile ndiye *aliyepewa jukumu la kutufasiria na kutufafanulia aya zake katika yale ambayo tunakhtalifiana*, kama iliovyoelezwa katika Sura 16:44 na 64.

b. Ni kwa sababu Mwenyezi Mungu na yeye (Mtume Muhammad (s.a.w.w.)) ndio waamuzi wetu wa mzozo wowote unaotutokea, ukiwemo huu wa *ahlul bayt* – katika hii Sura 33:33 - kuwa **ni** nani, **si** nani. Kwa hivyo, kama tunamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, hatuna khiyari ila kufuata uamuzi wao. (Sura 33:36).

Tatu: Bwana Mtume (s.a.w.w.), katika Hadith sahihi tulizotangulia kuzinukuu humu (uk. 6-7), tayari ashatufafanulia kuwa *ahlul bayt* waliokusudiwa katika Sura 33:33 **ni** nani, **si** nani. **Ishitoshe!** Akachukua *al-kisaa* (kishamia au shuka au guo), akajifinika yeye na wao – **bila ya kumwingiza mke wake yoyote** – na kusema kuwa *ahlul bayt* wake ni hao, halafu akawaombea Mungu. **Ishitoshe!** Na mmoja wa wake zake, aliyekiitwa Ummu Salamah – ambaye aya hii iliteremshwa nyumbani mwake – alipoomba aingizwe katiak hilo guo, Mtume (s.a.w.w.) **hakumkubalia!** Na juu ya yote hayo, ili kuzidi kuikokoteza tafsiri yake hiyo, ikawa kila asubuhi endapo msikitini kuswali hupitia mlango wa nyumba ya Imam Alii na Bibi Fatima na kuwandia: "Swalaa! Swalaa enyi *ahlul bayt*! Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu, enyi *ahlul bayt*, na kuwatakasa kabisa kabisa." (Sura 33:33).

Suali zetu hapa ni hizi: Kama maana ya neno *ahlul bayt* ni "wake wa Mtume" katika aya hii, kwa nini Mtume (s.a.w.w.) asiwaingize katika hilo guo lake? Kwa nini alipokuwa akenda msikitini, hakuwa akiwapitia

wakeze milangoni mwao nalhali walikuwa na majumba yao (Sura 33:33 na 34), na kuwanadia swala na kuwasomea aya hiyo, kama alivyofanya kwa nyumba ya Imam Alii na Bibi Fatima?

Baada ya ushahidi wote huu, bado Sheikh Mazrui anataka tuuvunje au tuukatae kwa kanuni za kilugha au usuli kana kwamba Bwana Mtumme (s.a.w.w.) hakizijua?! *Astaghfirullah*!

Tunavyosema na Tusivyosema

Katika uk. 61-63 Sheikh Mazrui amesema kwamba 'Shia wao hawakubali kwamba Aya hio inawaingiza wake wa Mtume (s.a.w.w.) katika AHLU AL-BAIT, na sababu zao – kama tulivyosema – ni mbili:

"1) Hoja ya kilugha. Na ufupisho wake ni kuwa *dhamiri* (*pronoun*) hapa ni ya kiume: sio ya kike. Kwa hivyo wahubiriwa si wake wa Mtume (s.a.w.w.).

"2) Riwaya zilizokuja kuhusu Aya hii zimewatoa wake wa Mtume (s.a.w.w.) katika jumla ya AHLU AL-BAIT

"Hizi ndizo hoja zao ambazo kwazo wamewatoa wake wa Mtume (s.a.w.w.) katika jumla ya AHLUL BAYT.

Majibu Yetu:

Hujja yetu kubwa ya kutowaingizia wake wa Mtume (s.a.w.w.) katika neno *ahlul bayt* la Sura 33:33 ni hiyo Na. 2 hapo juu: Kwamba Bwana Mtume (s.a.w) *yeye mwenyewe* amewatoa, kama riwaya k.w.k. (tiz uk. 6-7 humu) zinavyolishuhudia hilo.

Hilo la Na. 1 hapo juu – la dhamiri (*pronoun*) – shekhe wetu huyo ametupoteolea hujja yetu. Kwa hivyo ni bora hapa niirudie hujja hiyo japo kwa ufupi ijapokuwa, kabla ya hapa (uk. 15-19 humu), nishaieleza kwa urefu. Nayo ni hii:
Sibaaq ya aya yenye neno *ahlul bayt* (Sura 33:33) imeanzia aya ya 28 mpaka sehemu ya kwanza ya aya hiyo ya 33; na **zote** hizo zimewahubiria wake wa Mtume (s.a.w.w.) kwa dhamiri ya kike. Kisha ikafuatia *siyaaq* yake kwenye aya ya 34 ambayo **vile vile** wamehubiriwa wake wa Mtume (s.a.w.w.) kwa dhamiri ya kike.

Suali yetu hapo ikawa ni: Kama *sibaaq* na *siyaaq* ya aya hiyo yenye neno *ahlul bayt* zimekuja kwa dhamiri ya kike, kwa nini hapo katikati isendelee vivyo hivyo kwa dhamiri ya kike? Sababu yake, kwa hujja yetu, ni ile tuliyouieleza uk. 18 humu. Tafadhali isome tena.

Lakini Sheikh Mazrui ametupa mhadhara mrefu wa neno *ahl* kuwa ni kiume (uk. 62-65) ndiyo ikatumika dhamiri ya kiume, na (uk. 64) kuwa katika hilo neno lenyewe la *ahlul bayt* "Mtume mwenyewe (s.a.w.w.) anaingia." Ndipo ikatumika dhamiri ya kiume.

Majibu Yetu:

Hujja yetu hapa si uke wala uume wa neno *ahl* wala *ahlul bayt*. Hilo li mbali. Hujja yetu khaswa ni: baina ya aya zilizoitangulia sehemu ya aya yenye neno *ahlul bayt* – ambazo **zote** zimekuja kwa dhamiri ya kike - na ile iliyofuatia aya hiyo – ambayo **nayo pia** imekuja kwa dhamiri ya kike – kwa nini Bwana Mtume (s.a.w.w.) akaiweka aya hiyo ya kutumia dhamiri ya kiume?

Mbali ya uchambuzi mrefu wa kinahau aliotuolea shekhe wetu huyo (uk. 64-65) – ambao haujajibu suali yetu ambayo sisi wenyewe humu tushaijibu kwenye uk. 18 – **kwa mara ya kwanza** ameongeza hujja ya kwamba hilo neno *ahlul bayt* la Sura 33:33 si la wake zake peke yao, bali "na Mtume aingia" (tiz. uk. 64 wa kitabu chake), ndio ikatumiwa dhamiri ya kiume!

Tunasema **kwa mara ya kwanza** kwa sababu kabla ya ukurasa huo, **hatukuona popote** amemtia Mtume (s.a.w.w.). Tulioliona ni kuwa kote kote amewakhusu wake zake tu. Kwa mfano, tiz. uk. 44, 49, 61 wa kitabu chake.

La kushangaza hapa ni kwamba Sheikh Mazrui ameamua kuikataa tafsiri yetu ya *ahlul bayt* na Hadith za Mtume (s.a.w.w.) tulizozitegemea – ambazo pia zinakubaliwa na wanavyoni wakubwa wakubwa wa kisunni – kwa kutmia hujja za *sibaaq* na *siyaaq*, kanuni za kiusuli na za kilugha, kana kwamba hao wanavyoni wa kishia na wa

kisunni hawazijui au hawajazitia maanani hujja hizo!! Hata mahali pamoja hakujasiri kutunukulia "Hadith ya Mtume" inayotolewa na kutegemewa na wanaoshikilia kuwa makusudio ya neno *ahlul bayt* ni "wake zake." Inshallah katika sura inayofuatia hii tutaitoa riwaya yake na kueleza sababu zetu za kuikatalia ambapo kwenda msomaji wetu akaelewa – khaswa baada ya kujua kuwa Sheikh Mazrui ni wa madhihabi ya Ibadhi – kwa nini hakupendelea kuitumia!

Kiini cha Mjadala Wetu

Hata hivyo, kabla ya kuzichambua Hadith zitumiwazo kuthibitisha kwamba neno *ahlul bayt* lina maana ya "wake wa Mtume (s.a.w.w.)"; na kabla ya kulijadili neno *ahl* lililomo katika Sura 28:29 ambalo Sheikh Mazrui amelitumia (uk. 65 wa kitabu chake) kutolea hujja kuwa lina maana ya *mke*, ni muhimu sana tuelewe kwanza *ni nini khaswa kiini cha mjadala wetu*.

Kiini cha mjadala wetu *si* maana ya neno *ahl* au *ahlul bayt* kama lilivyokuja katika aya k.w.k za Qur'ani. Kiini ni: *ni nini muradi wa neno ahlul bayt lililomo katika Sura 33:33*, **si penginepo**. Kwa nini?
Kwa sababu:

1. Tafsiri ya Mtume (s.a.w.w.) ndiyo inayowekwa mbele ya tafsiri zozote zile, ya yoyote yule (kama tulivyokwisha kuona humu), kwa kuwa yeye ndiye aliyepewa jukumu la kutufasiria hii Qur'ani (Sura 16:44).

2. Mtume (s.a.w.w.), kwa Hadith zilizo sahihi, zilizokubaliwa na wanavyuoni k.w.k wa Tafsir na Hadith[4], amesema kuwa waliokusudiwa kwa neno *ahlul bayt* **katika Sura 33:33** ni hawa watano tuliowataja sisi. *Wake zake hawamo*!

3. Tafsiri yoyote nyengine isiyowafikiana na ile ya Mtume (s.a.w.w.) – kwa kutumiliwa hujja za kiusuli, lugha, *sibaaq* na *siyaaq*, n.k. - ni sawa na kumfanya Bwana Mtume (s.a.w) ni mjinga wa hayo!

4 Haya utayapata katika *Tafsir Twabari*, *Durrul Manthur* ya Suyuutwi, *Sunan Tirmidhi*, *Sahih Muslim*, na vinginevyo.

Ili kutimiza hujja, hebu tutizame neno *ahl* ambalo Sheikh Mazrui amelitumia katika uk. 65 wa kitabu chake kutolea hujja kuwa lina maana ya *mke*. Jee, neno hilo lina maana hiyo hiyo kila lilipotumiwa katika aya nyengine? Tuangalie, kwa mfano, Sura 29:33 yenye maneno ya malaika kumwambia Nabii Lut: "Hakika sisi tutakuokoa wewe na *ahl* zako, isipokuwa *mkeyo*, aliye miongoni mwa watakaokaa nyuma." Jee, neno *ahl* hapo lina maana ya *mke*? Kama ni hivyo jee, itakuwa sawa kuifasiri aya hiyo kwa: "Hakika sisi tutakuokoa wewe na *mke wako*, isipokuwa *mkeyo*, aliye miongoni mwa watakaokaa nyuma"?!! Lizingatie hilo, ndugu msomaji.

Au katika Sura 11:45 pale Nabii Nuh aliposema: "Ewe Mola wangu! Hakika mwanangu ni katika *ahlii…*" Jee, ni sawa kuifasiri aya hiyo kwa: "Hakika mwanangu ni katika *wake* zangu"?!! kwa kuwa neno *ahl*, katika aya nyengine, limekuja kwa maana ya *mke*, na kwa kuwa Qur'ani hujifasiri yenyewe kwa yenyewe? Lizingatie na hilo pia, ndugu msomaji.

Tuangalie na mfano mwengine: wa neno *swaahib*. Katika Sura 9:40 neno hilo limetumiwa kwa mtu maalumu aliyekuwa pangoni pamoja na Mtume (s.a.w.w.) *ijapokuwa halikutajwa jina lake katika Qur'ani*. Na katika Sura 18:34 neno hilo (*waqaala liswaahibihii*) limetumiwa kwa mtu mwengine *ambaye pia hakutajwa jina lake*. Lakini wanavyuoni wa Tafsir wanatwambia kuwa *swaahibihii* ya Sura 9:40 haina muradi mmoja na ule wa Sura 18:34 nalhali neno lililotumiwa ni lilo hilo moja. Wameujuaje muradi wazo, kuwa wa aya moja **sio** ule ule wa aya nyengine. Jee, si Qur'ani hujifasiri yenyewe kwa yenyewe?

Tuje kwenye matumizi ya lugha. Jee, twaweza kutumia kanuni zake *mara zote* kukosolea yaliyokuja katika baadhi ya aya za Qur'ani na/au baadhi ya tafsiri za Mtume (s.a.w.w.)? Hebu tuangalie mifano miwilli mitatu tu ya Sura 3:61 ijulikanayo kwa jina la *ayatul mubahalah* (aya ya kuapizana). Aya hiyo yasema hivi: "Na atakayehujiana na wewe katika hilo baada ya ujuzi uliokujilia, wambie: Njooni tuwete *watoto wetu* na watoto wenu, na *wanawake wetu* na watoto wenu, na *nafasi zetu* na nafsi zenu; kisha tuombe kwa kunyenyekea tujaalie laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie wenye kusema uwongo."

Wanavyoni wa Tafsir na Hadith wanatueleza kuwa aya hii iliteremshwa kumwamrisha Mtume (s.a.w.w.) kwamba: iwapo hao wanaojiita wakristo watahujiana naye juu ya khabari ya Nabi Isa (a.s.), wasikubali yaliyokuja katika Qur'ani, basi awete watoke (wao, watoto wao na wanawake wao) na Mtume naye atoke (wao, watoto wao na wanawake wao), wasimame mahali pamoja, kisha wamwombe Mwenyezi Mungu awateremshie laana walio waongo kati ya makundi mawili hayo.

Maneno matatu yaliyomo katika aya hiyo – *abnaa–anaa* (watoto wetu), *nisaa-ana* (wanawake wetu), na *an-fusanaa* (nafsi zetu) – **kilugha** yaeleweka vizuri. Lakini jee, Bwana Mtume (s.a.w.w.) aliyafasiri maneno hayo *kilugha*? Jawabu ni: *naam* na *la*! Yale ya upande wa Wakristo ni *naam*, lakini yake ya upande wake ni *la*! Vipi?

Hivi! Hadith sahihi zilizonukuliwa katika vitabu vya baadhi ya wanavyuoni wa Hadith *wasio* mashia[5], *bali wengine wapinzani wa mashia kamwe*[6], vyasema kuwa upande wake wa *abnaa-anaa* Mtume (s.a.w.w.) aliwaleta Hasan na Husein. Lakini hao hawakuwa ni watoto wake; walikuwa ni wajukuu zake. Kwa lugha ya Kiarabu lingetumika neno *ahfaadanaa*, tena si kwa *jam'u* (wingi) bali kwa *muthanna* (ya watu wawili). Upande wake wa *nisaa-anaa* hakumleta mke wake *hata mmoja*, bali alimleta Bibi Fatima ambaye **si** mke wake bali binti yake! Huyo, kwa lugha ya Kiarabu, haingii katika *nisaa*; ni *bint*. Na upande wake wa *an-fusanaa* alimleta Alii b. Abii Twalib *peke yake*; hakumleta *swahaba yoyote mwengine* – Si Abu Bakar wala Umar wala Uthman! Kisha, baada ya kuwakusanya hao akasema: *Haa ulaai ahlii* (hawa ni *ahl* wangu)!!

Ndugu msomaji! Tizama hapo jinsi Mtume (s.a.w.w.) alivyotumia neno *ahl* kuelezea watu hao. Jee hao walikuwa "wake zake" **kwa sababu tu** ya kuwa neno *ahl*, katika lugha ya Kiarabu, huja pia kwa maana hiyo? Ukumbuke pia kwamba, katika kutueleza muradi wa neno *ahlul bayt*

5 Hayo nayo utayapata katika Tafsir kubwa za Qur'ani za wasio Shia.

6 Hili pia ni kama Na. 5 hapo juu

katika Sura 33:33 – ambalo ndilo tunalolikadili katika kitabu hiki – Bwana Mtume (s.a.w.w.), **kwa watu hao hao** alisoma *haa ulai ahlii*, amesema: *Haa ulaai ahlu baytii*. Jee, na hapo pia, Bwana Mtume (s.a.w.w.) alilitumia neno *ahlul bayt* kwa maana ya "wake" **kwa sababu tu** maneno mawili hayo, mahali pengine huja kwa maana ya "mke" au "wake"? Majibu ni: La! Kwa sababu tunazozieleza hapa chini.

Matumizi ya Maneno Katika Lugha

Maneno ya lugha yoyote – yawe ni ya Kiarabu au lugha yoyote nyengine – kwa kawaida hayawi na maana moja ile ile kile mahali. Maana yake hutegemea neno hilo limetumiwa vipi na katika fuo (*qarina/context*) gani la maneno. Limetumiwa kilugha ya kawaida? Au kifiqhi/kisharia? Au kistilahi (*conventional/technical*)?

Tuchukue, kwa mfano, hili hili neno *ahlul bayt*. Kilugha, ni kweli neno linaweza kuwa na maana ya mke au wake wa nyumba fulani. Lakini, kama wanavyoeleza wana-kamusi wa lugha ya Kiarabu[7], neno hilo vile vile – zaidi ya "wake" – lina maana ya wowote wanaokaa katika nyumba hiyo: wawe ni jamaa wa mume au mke wa nyumba hiyo, wageni walioshukia nyumba hiyo; watumishi wa nyumba hiyo, n.k.

Kifiqhi au kisharia, linapotumiwa kwa mfano kwa muktadha wa mas'ala ya zaka, lina maana ya wale walioharimishwa kupokea zaka. Hao ndio wale waliotajwa na Zayd b. Arqam katika Hadith iliyomo katika *Sahih Muslim*, ijapokuwa hakuwataja wote. Litumiwapo hivyo, neno *ahlul bayt* haliwezi kuwa na maana ya "wake wa Mtume (s.a.w.w.)" kwa sababu wao *si haramu kwao* kupokea zaka.

Hali kadhaalika tunapokuja *kiistiilahi*; huwa na maana mbali, isiyo ya kilugha wala wa kifiqhi **kwa sababu kubwa** kwamba *hivyo ndivyo alivyolifasiri Bwana Mtume (s.a.w.w.)* aliyepewa jukumu la kutufasiria Qur'ani, kama tulivyokwisha kuona katika kurasa zilizopita humu. Kwa kuwa Bwana Mtume (s.a.w.w.) amelifasiri neno hili **katika Sura 33:33**

7 Kama vile *Lisaanul Arab*, *Mu'jamu Maqaayiisil Lugha*, *al-Mufradaat*, *al-Qaamus al-Muhit* katika kulieleza neno *ahl*.

kwa maana hii tuliyoieleza sisi humu, hatuwezi – *kama waislamu* – kuikosoa au kuikataa tafsiri hiyo *kilugha* au *kifiqhi*. Maana tukifanya hivyo tutakuwa – Mwenyezi Mungu atuepushe na hilo – ni sawa na kusema kuwa Bwana Mtume (s.a.w.w.) hakiyajua hayo!!

Kwa hivyo, *njia ya pekee* iliyobakia ya kuikosoa au kuikataa tafsiri hiyo ni kuthubutisha kwamba hizo Hadith tulizozinukuu kusema kuwa hivyo ndivyo alivyosema Bwana Mtume (s.a.w.w.) ni za *uwongo* au *si sahihi*. **Hilo Sh. Mazrui hajaweza kulifanya!**

Kujeruhi Sanad

Aliloweza kulifanya ni kuzijeruhi baadhi ya sanad za baadhi ya Hadith tulizozitolea ushahidi sisi, zikiwemo sanad 16 za ile Hadith ya Vizito Viwili ambazo tumezijibu katika uk. 16-39 wa kitabu chetu kiitwacho *Hadith al-Thaqalayn: Hadith Sahihi*. Kwa kuwa uslubi aliokwenda nao kujeruhia sanad za Hadith zinazotumiwa kufasiria Sura 33:33 ni kama ule alioutumia kujeruhia *Hadith al-Thaqalayn*, sioni tena dharura ya kuzitetea sanad hizo kama nilivyofanya kule. Hapa majibu yangu ni haya ambayo nakuomba ndugu msomaji uyazingatie.

Majibu Yetu:

Walioandika khabari za wapokezi wa Hadith, ambao Sheikh Mazrui ametegemea vitabu vyao kujeruhia sanad zao, *ndio wale wale* ambao (baadhi yao) wamesema kuwa Hadith hizo *ni sahihi*, kama tulivyotangulia kudokeza humu. Jee, mbona wao wamezikubali Hadith hizo pamoja na kujua kuwa, katika sanad zao, mna watu ambao walivyowaeleza katika vitabu vyao, kumempa hujja Sheikh Mazrui kuzikataa Hadith hizo. Jee hapa tufuate ya nani? Tufuate ya wanavyoni wa Hadith – ambao ndio wataalamu na mabingwa wa fani hiyo – au ya Sheikh Mazrui, ambaye ni shekhe wa kawaida tu; si mwanachuoni wa Hadith? Hilo nnakuachia wewe, ndugu msomaji, uliamue.

Sasa, katika sura inayofuatia, tuangalie mategemeo ya wanaosema kuwa *ahlul bayt* ni "wake wa Mtume (s.a.w.w.)". Jee, mategemeo yao yana mashiko?

WAKE WA MTUME WAMO?

Mpaka hapa tushaona kwamba, kwa mujibu wa Hadith **sahihi** za Bwana Mtume (s.a.w.w.), muradi wa neno *ahlul bayt* katika **Sura 33:33** ni yeye mwenyewe Mtume (s.a.w.w.), Alii b. Abi Twalib (a.s.), Hasan b. Alii (a.s.), Husein b. Alii (a.s.), na Fatima bt. Rasulillah (a.s.). Lakini Sheikh Mazrui haikubali tafisri hiyo! Yeye ameshikilia kuwa muradi wa neno hilo katika aya hiyo ya sura hiyo ni "wake wa Mtume;" na ametoa hujja k.w.k katika kitabu chake (uk. 46-66) kutilia nguvu dai hilo, ambazo nasi tushazijibu humu (uk. 14-32). Hata hivyo, la kushangaza hapa ni kwamba – *hata mahali pamoja* katika kitabu chake – hakuzitolea ushahidi zile riwaya ambazo wenziwe wenye maoni kama yake huzitegemea! Lakini sisi, hapa chini, tutazitaja na kutoa sababu zetu za kuzikatalia. Ksha nitakuachia wewe, ndugu msomaji, uamue!

Riwaya Wanazozitegemea

Riwaya zenyewe ni zile zilizosimuliwa na watu wane:

1. Ibn Abbas
2. Ikrimah
3. Urwa b.Zubayr
4. Muqatil b. Sulayman

Mbali na kuwa riwaya za watu wane hao zinapingana na zile zilizo *sahihi* na *mutawatir* zilizosimuliwa na maswahaba k.w.k. wakubwa wakubwa – tulizotangulia kuzitaja na kuishiria humu vitabu ziwezamo kupatikana – hali kadhaalika hazikubaliki kwa sababu tutakazozitoa hapa chini, kwa kuwachambua mmoja baada ya mmoja ya watu wane hao. Tuanze na:

1. Ibn Abbas

Huyu jina lake kamili ni Abdallah b. Abbas b. Abdul Muttalib. Alikuwa binami yake Mtume (s.a.w.w.) na mmoja kati ya maswahaba wake maarufu.

Katika *Tafsir Ibn Kathir* na *Tafsir al-Twabarii* mna riwaya isemayo kuwa imepokewa kwa Ibn Abbas kuwa amesema kwamba muradi wa neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 ni "wake wa Mtume (s.a.w.)"!! Hilo halikubaliki kwetu kwa sababu zifuatazo:

a. Bwana yuyu huyu ana riwaya nyengine zilizo sahihi *zinazopingana* na riwaya hii, kama ile tuliyoitaja humu (uk. 7) ya kumwona Mtume (s.a.w.w.) akipitia nyumba ya Alii na Bibi Fatima kwa miezi tisa, kila alipokuwa akenda msikitini, na kuwanadia swala na kuwasomea Sura 33:33. Pia ile riwaya yake nyengine ambayo ni *muttafaqun 'alayhi*[1] inayosema hivi: "Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwamba Mwenyezi Mungu amewagawanya viumbe (Vyake) vigawanyo viwili; akaniweka mimi katika kigawanyo kilicho bora yavyo… Kisha akayafanya makabila ni majumba; akaniweka mimi katika bora ya majumba. Ndilo neno Lake (Mwenyezi Mungu s.w.t.): *Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu nyinyi ahlul bayt, na kuwatakasa kabisa kabisa*."

b. Ana riwaya nyengine ambamo yumo mtu aitwaye Ikrimah ambaye, kama tutakavyoona hapo chini, ni **mwongo asiyeaminika!**

2. Ikrimah

Huyu ni mtu aliye maarufu kwa jina la Ikrimah *mawlaa* (huru la) Ibn Abbas tuliyemweleza hapo juu. Yeye **hakuwa swahaba**. Alikuwa *taabi'i*, kizazi kilichokuja baada ya maswahaba. Kwa hivyo **hakumwona kabisa Mtume (s.a.w.w.)!**

Kama ni hivyo basi, vipi tutaikubali riwaya yake inayosema kwamba yeye (Ikrimah) *amempokwa* Mtume (s.a.w.w.) akisema kuwa muradi wa neno *ahlul bayt* katika Sura 33:33 ni "wake zake khaswa"? Amempokea wapi naye hakukutana naye? Hicho si kioja?

Hata ile riwaya yake nyengine, isemayo kwamba yeye Ikrimah

1 Riwaya ambayo ni *muttafaqun 'alayhi*, kwa ndugu zetu wa kisunni, ni ile ambayo Bukhari na Muslim wamekomangana kuwa ni sahihi

amempokea Ibn Abbas kwamba Mtume (s.a.w.w.) amesema hivyo, **pia haikubaliki** kwa sababu (a) tulizokwisha kuzitaja hapo juu kuhusu Ibn Abbas, na (b) Ikrimah akijulikana kuwa mwongo asiyeaminika. Kwa mfano, inaelezwa kwamba wakati mmoja alionekana amefungwa kwenye mlango na Alii mtoto wa Ibn Abbas. Alipoulizwa kwa nini amemfanya hivyo, Alii alijibu, "khabithi huyu *amsingizia uwongo* babangu."[2]

Ili kumjua zaidi mtu huyu, na kujua kwa nini sisi hatuwezi kuzikubali riwaya zake, hebu - japo kwa mukhtasari – tutizame wanavyuoni na wataalamu wa Hadith wamemwelezaje katika vitabu vyao:

Alikuwa Ikrimah ni katika makhawarij.[3]

Alikuwa na maoni ya kiIbadhi.[4]

Alikituhumiwa kuwa yu mwongo![5] Na kisa chake tulichokitaja hapo juu, cha kumsingizia Ibn Abbas uwongo, ni mashuhuri sana.[6]

Hayo ni kwa mukhtasari tu. Kwa wale ndugu zetu wajuwao Kiarabu, naomba wayasome zaidi ya hayo, ya mtu huyu, katika vitabu nilivyovitaja katika kidokezo cha saba mwisho wa sura hii.[7]

Huyo ndiye Ikrimah, na hizo ndizo sababu zetu za kutozikubali riwaya zake.

3. Urwa b. Zubayr

Huyu babake ni Zuhayr b. al-Awwaam, mmoja wa maswahaba wa Mtume (s.a.w.w.); na mamake alikuwa Asmaa bt. Abu Bakar, dadake Bibi Aisha bt. Abu Bakar, mke wa Mtume (s.a.w.w.). Kwa hivyo Bibi Aisha alikuwa khalati yake. **Yeye hakuwa swahaba. Kwa hivyo**

2 Haya yote utayapata katika vitabu vya *rijaal* (wapokezi wa Hadith k.v. *Siyaru A'alaamun Nubalaa* na *Mizaanul I'itidaal* vya Imam Dhahabii).

3 Hili pia ni kama Na. 2 hapo juu

4 Hili pia ni kama Na. 2 hapo juu

5 Hili pia ni kama Na. 2 hapo juu

6 Hili pia ni kama Na. 2 hapo juu

7 Hili pia ni kama Na. 2 hapo juu

hakumwona Mtume (s.a.w.w.). Kama Ikrimah hapo juu, alikuwa *taabi'i*.

Riwaya yake kwetu **haikubaliki** kwa sababu mbili:

a. Ni *mawquuf*; yaani ni riwaya ambayo sanad yake huishia kwa swahaba au maswahaba, haiendelei mbele.

b. Alikijulikana kwamba alikuwa adui wa Alii, Fatima, Hasan na Husein (a.s.). Pia akituhumiwa kwa kumvutia fadhila khalati yake, Bibi Aisha, aliyekuwa mpinzani mkubwa wa Imam Alii (a.s.).

4. Muqatil b. Sulayman

Huyu naye, kama wenziwe hapo juu, riwaya yake **haikubaliki** kwa sababu zifuatazo:

a. Alikuwa "mwongo na jasiri."
b. Hadith zake ni "za kuachwa"
c. Alikuwa "*mushabbih*", mwenye kumfanaisha Mwenyezi Mungu na viumbe Vyake!
d. Alikuwa "akipokea kwa mayahudi na manasara ilimu ya Qur'ani inayokubaliana na vitabu vyao."
e. Alikuwa akiwambia watu wamuulize wanachotaka ili awajibu, isipokuwa *arsh*. Akaulizwa: "Ni nani aliyekinyoa kichwa cha Adam alipohiji kwa mara ya kwanza?" Akajibu: "Sijui."
f. Imepokewa tena kwamba alisema maneno kama hayo alipokuwa Makka. Mtu mmoja akamjibu: "Nieleze kuhusu chungu; chango zake zipo wapi?" Akanyamaza!

Mpaka hapa tushaziona sababu zetu – japo kwa mukhtasari – za kukatalia riwaya za kusema kuwa muradi wa neno *ahlul bayt* katika **Sura 33:33** ni "wake wa Mtume (s.a.w.w.)". Sasa ni juu yako, ndugu msomaji, kuamua la sawa ni lipi: baina ya tunayosema sisi mashia na *jumhur* ya wanavyuoni wa kisunni, na anayoyasema Sheikh Mazrui na wapinzani wengine wachache wa *ahlul bayt* kama tulivyowaeleza sisi.

TULIYOYAJADILI HUMU KWA MUKHTASARI

Msingi wa mjadala wetu katika kitabu hiki ni muradi wa neno *ahlul bayt* katika **Sura 33:33**; lina maana gani?

Kwa mujibu wa maelezo ya Sheikh Juma M. Al-Mazrui, katika kitabu chake alichokiita "*Al-Qistasu Al-Mustaqim: Mezani ya Haki*", na kufuatana na imani ya madhihabi yake ya Ibadhi, neno hili katika aya hiyo lina maana ya "wake wa Mtume (s.a.w.w.)." Sisi nasi, kwa upande wetu kama mashia, tumeyakataa maelezo hayo. Tumeshikilia kwamba, kufuatana na imani ya madhihabi yetu, neno hili katika aya hiyo lina maana ya "Bwana Mtume (s.a.w.w.) pamoja na Alii b. Abi Twalib, Fatimah bt. Rasulillah, Hasan b. Alii na Husein b.Alii".

Kutilia nguvu dai lake, Sheikh Mazrui ametoa hujja alizoziita (uk. 49) "misingi ya kufasiria (Qur'ani)" na kuzitolea maelezo marefu, kuanzia uk. 46-66. Lakini *hata mahali pamoja* hakututajia **msingi mkubwa na wa mwanzo** wa kufasiria Qur'ani, ambao ni *Mtume (s.a.w.w.) ameifasiri vipi aya hiyo*.

Kwa upande wetu, kabla ya kuzijibu hijja zake hizo, tumemkumbusha kwamba **msingi wa kwanza** wa kufasiria Qur'ani ni Hadith za Mtume (s.a.w.w.) (uk. 12 humu) na kwa nini iwe hivyo. Hilo yeye kwa bakhti mbaya, amelisahau au amelipuuza! Tukampa ushahidi wa mashekhe *wasiokuwa mashia* waliosema hivyo pia (uk. 13 humu)!

Baada ya hilo tukamnukulia Hadith k.w.k. za Mtume Muhammad (s.a.w.w.) zinazosema hivi tusemavyo sisi, mashekhe waliozikubali riwaya hizo kuwa ni sahihi na baadhi ya vitabu vya Tafsir na Hadith vilimotajwa riwaya hizo. Wala hatukuzitoa Hadith hizo katika vitabu vya kishia kwa kujua kwamba, kwa chuki na upinzani alionao Sheikh Mazrui dhidi ya ushia na mashia, hatazikubali. Bali tumezitoa katika vitabu vya kisunni ambao, kwa kutaka kuuficha uibadhi wake, Shekhe wetu huyo amejaribu kujinasibisha nao!


Kisha ndio tukazijibu hujja zake alizozitoa kutetea dai lake (uk. 14-32 humu) moja baada ya moja.

Baada ya kuzijibu hujja zake hizo, ndipo tulipomalizia (uk. 33-38 humu) kitabu chetu hiki kwa kuzijeruhi zile sanad za riwaya zinazotegemewa na wenzake walio na msimamo kama wake – wa kuwa *ahlul bayt* waliotajwa katika Sura 33:33 *ni wake wa Mtume (s.a.w.w.)* – ijapokuwa yeye hakutudondolea *riwaya nyengine zisizokuwa hizo* alizozitegemea yeye!

Hiki ni cha pili katika mfululizo wa vitabu vilivyokusudiwa kujibu shutuma na madai ya Sheikh Juma Moh'd Al-Mazrui dhidi ya itikadi na imani za Shia Ithna-ashariyya aliyoyaandika katika kitabu chake alichokiita *Al-Qistasu Al-Mustaqim* (*Mezani ya Haki*).

Katika kitabu hiki Sheikh Abdilahi Nassir anayajibu yale yaliyoandikwa na Sheikh Al-Mazrui katika Sura ya Tatu na ya Nne ya kitabu chake hicho (uk. 43-114) ya kudai kwamba muradi wa neno ***ahlul bayt*** katika Sura 33:33 ni "wake wa Mtume (s.a.w.w.)" si "***ahlul-kisaa***" kama walivyoshikilia machia na wengi sana wa wanavyuoni wa kisunni.

Ameyajibu hayo kwa kuzijadili kiilimu na kimantiki hujja alizozitegemea Sheikh Al-Mazrui za "sibaaq na siyaaq, kanuni za kiusuli na hujja za kilugha"



AHLUL BAYT CENTRE
S.L.P. 84603 - 80100
MOMBASA, KENYA